
*Jarida Toleo la Aprili - Juni* 2022/2023

TANZANIA IMARA KAZI IENDELEE

# FAHARI YETU
## HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

MERU DC KAZI IENDELEE | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI | JARIDA LA APRILI- JUNI




**JARIDA 2022/2023**
**TOLEO LA APRILI-JUNI**

HALIUZWI

Imeandikwa na Kutolewa na;
Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Wilaya ya Meru

Mhariri Mkuu: Zainabu J. Makwinya
Mhariri Msaidizi: Annamaria Makweba
Msanifu wa Jarida : Ludovick Mkenda
Msanifu Msaidizi : Issaya Sango


Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Meru
S.L.P 462
Usariver
Simu: +255272970482
Barua pepe: ded@merudc.go.tz
www.merudc.go.tz

# UTANGULIZI



Mwl. Zainabu J. Makwinya
Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Meru

Halmashauri ya Wilaya ya Meru ipo Mashariki mwa mkoa wa Arusha na imelala kati ya latitudi 36o43'16" na 37o 03'43"; na Longitudi -3o04'30" na -3o35'28". Halmashauri ya Wilaya ya Meru inapakana na Wilaya ya Longido kwa upande wa Kaskazini, Wilaya za Siha na Hai kwa upande wa Mashariki (Mkoa wa Kilimanjaro), Wilaya ya Simanjiro kwa upande wa Kusini (Mkoa wa Manyara), na Wilaya ya Arusha na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kwa upande wa Magharibi. Halmashauri ya Meru ni miongoni mwa Halmashauri 7 zinazounda Mkoa wa Arusha. Halmashauri ya Meru imetokana na kugawanywa kwa iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru na kuwa Halmashauri mbili za Wilaya za Meru na Arusha. Halmashauri ina jumla ya Madiwani 35, kati ya hao, Madiwani 26 ni wa kuchaguliwa na Madiwani 9 ni wa Viti Maalum. Naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuleta fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Halmashauri ya Wilaya ya Meru imeendelea kutekeleza shughuli za Miradi ya maendeleo katika sekta mbalim bali kama ambavyo Serikali ya Awamu ya sita inavyofanya juhudi



Mhe. Jeremia Kishili
Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Meru



Mhe. Emmanuela Kaganda
Mkuu wa Wilaya ya Arumeru

kuhakikisha inaleta fedha katika Halmashauri zote nchi ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi. Halmashauri ya Wilaya ya Meru imetoa jarida la Fahari yetu toleo la Nne kwa kipindi cha Mwezi Aprili hadi Juni 2023 ili kuonyesha kazi zilizofanyika kwa kipindi cha miezi mitatu katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Karibuni msome Jarida la Fahari yetu la Halmashauri ya Wilaya ya Meru, lenye kuonyesha kazi na shughuli mbalimbali zilizofanywa katika kipindi cha hicho.


## YALIYOMO


01 Uzinduzi wa Jengo la dharura

03 Mwenge wa Uhuru

06 Klabu za watoto watembelea Bungeni.

08 Dc Arumeru ashiriki katika ujenzi wa madarasa.


09 Uteketezaji hekari za bangi

10 Utatuzi wa Miundombinu chakavu meru

11 Upandaji wa miti

13 Ziara ya Kamati ya fedha mipango na utawala .

14 Umisseta.


# FAHARI YETU

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, S.L.P 462, Usa River, Arusha, simu +255272970482, Barua pepe: ded@merudc.go.tz, www.merudc.go.tz



**MAKAMU WA RAIS Dkt. MPANGO AZINDUA JENGO LA DHARURA HOSPITALI YA WILAYA ARUMERU**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa madaktari na watoa huduma wote kuendelea kufanya kazi kwa kujituma ,upendo, kujitoa na kuzingatia weledi na maadili ya tasnia hiyo utabibu ili kuokoa maisha ya watanzania Makamu wa Rais amesema hayo wakati wa ufunguzi wa jengo la huduma ya dharura EMD katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mkoani Arusha, amesema viongozi wa hospitali hiyo wanapaswa kutoa umuhimu mkubwa katika kutunza vifaa tiba kwa kuhakikisha vinafanywa ukarabati wa wakati ili vidumu kwa muda mrefu. Aidha, ameongeza kwamba seri kali ya awamu ya sita itaendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya afya ili kuhakikisha watanzania wote wanapata huduma bora za afya na kwa ukaribu Zaidi Amesema Serikali inatarajia kukabidhi magari matatu, mawili yakiwa ni ya wagonjwa katika hospitali hiyo ya pamoja na watumishi wa afya zaidi ya 25 wakiwemo madaktari kwa Halmashauri hiyo ikiwa ni njia ya kukabiliana na changamoto za upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya Wilayani humo. Halikadhalika Makamu wa Rais ametoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto kuzingatia sheria za usalama barabarani li kuepukana na ajali za mara kwa mara zinazogharimu Maisha ya wananchi, Amesema asilimia kubwa ya wagonjwa wanaofikishwa katika huduma za dharura ni ajali hivyo amelisihi jeshi la polisi kusimamia sheria zilizowekwa kikamilifu ili kuendelea kupunguza adha ya ajali nchini. Aidha, Makamu wa Rais ametoa wito kwa wananchi wa Arumeru kuhakikisha wanatatua migogoro kwa njia ya amani na upendo na kuacha kujichukulia sheria mkononi ambazo husababisha madhara katika jamii kama vile majeruhi na vifo. umuhimu wa kuhudhuria kliniki kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ili kuepukana na changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa kujifungua.



**MAKAMU WA RAIS Mhe. Dkt. MPANGO AKIKABIDHIWA KAMBA YA KUFUNGA NG'OMBE KAMA ISHARA YA KUPOKEA ZAWADI YA NG'OMBE KWA RAIS Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN**

Kutokana na Maboresho Makubwa katika sekta za mbalimbali Wilayani Arumeru, yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wananchi wa Wilaya hiyo Wametoa zawadi ya Mtamba (ng'ombe) wawili kwa ajili ya Mheshimiwa Rais Samia na Makamu wa Rais Dkt. Mpango. Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda wakati akimkabidhi Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango Kamba Maalumu ikiwakilisha zawadi hizo, amesema Wananchi wa Arumeru wanampongeza Mhe. Rais kwani wamepokea fedha nyingi za maendeleo na wanajivunia kunufaika na utendaji wa awamu ya sita.

ikiwakilisha zawadi hizo, amesema Wananchi wa Arumeru wanampongeza Mhe. Rais kwani wamepokea fedha nyingi za maendeleo na wanajivunia kunufaika na utendaji wa awamu ya sita.

Mhe. Kaganda amebainisha Wilaya hiyo kupokea fedha nyingi ambapo kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Serikali ilitoa bilioni 1.9 za miundombinu katika sekta za Elimu na Afya, Bilioni 1.6 za urasimishaji Ardhi, Milioni 550 fedha za tozo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Mareu na ukamilishaji wa vyumba vinne vya madarasa katika shule za Sekondari umoja Kingori na Muungano, Milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la huduma za dharura ( EMD) katika Hospitali ya Wilaya ya Meru ambalo limezinduliwa leo. Milioni 509 za ununuzi wa vifaa tiba zikiwemo mashine za kisasa katika jengo la EMD.



# MIRADI YA MERU YAPITA KWA KISHINDO MBIO ZA MWENGE WA UHURU - 2023.



Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2023 zimeridhia na kupongeza Miradi 8 katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru yenye thamani ya shilingi Bilioni 8.6 Aidha, kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa Bw. Abdala Shaibu Kaim. ameweka mawe ya msingi kwenye miradi mitano ya, Ujenzi wa Barabara ya kiwango cha lami Sangisi - Ndoombo (mita 900) katika Kata ya Akheri, Ujenzi wa Kituo cha Afya Maroroni, Ujenzi wa Mradi wa Usambazaji maji Safi Imbaseni, Ujenzi wa kituo cha mafunzo kwa jamii Cha shirika lisilo la Kiserikali la Fondation for Tomorrow pamoja na shule ya Sekondari Precious Leaders katika Kata ya Malula. Vilevile mbio za Mwenge wa Uhuru Umetembelea, kukagua na kuridhia miradi mitatu ya kikundi cha vijana cha Agri Business Enterprises Katika Kata ya Seela -Singisi, Ukamilishaji wa ujenzi wa mnara wa tanki la Maji katika kituo cha afya Maroroni, utunzaji wa chanzo cha Maji na Hifadhi ya Mazingira Kibola katika Kata ya Nkoanekoli, Ikumbukwe Tarehe 29.06.2023 Halmashauri ya Wilaya ya Meru ilipokea Mwenge wa Uhuru kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, na kuukimbiza umbali km 115.9. Meru tupo vizuri na kazi iendelee



# MWENGE WA UHURU KUKIMBIZWA KM 115.9 KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru amepokea mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa Mwaka 2023, kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha Selemani Msumi, ambapo Mwenge huo umepita katika Tarafa Tatu (3) ambazo ni Poli, Mbuguni na King'ori, Pia Mwenge wa Uhuru umekimbizwa katika Kata 7 kati ya Kata 26 na katika Vijiji 7 kati ya vijiji 90 vinavyounda Halmashauri ya Wilaya ya Meru

Aidha, Mwenge wa Uhuru umekimbizwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, umbali wa Km 115.9 Mwenge huu umepita katika miradi nane (8) ambayo imekaguliwa, imezinduliwa, kuwekwa jiwe la msingi na kufunguliwa. Miradi hii imegusa sekta za Afya, Elimu, Maji, Barabara, na Kilimo yenye thamani ya shilingi 8,607,890,128.12. "Tunza Mazingira, Okoa Vyanzo Vya Maji Kwa Ustawi wa Viumbe Hai na Uchumi wa Taifa" Ndiyo kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru 2023.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl. Zainabu Makwinya akikabidhiwa Mweenge wa Uhuru kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha Eneo la Shangarai



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Longido Mhe Marko Ng'umbi soko la Oldonyosambu

# PICHA ZA MIRADI YA MWENGE WA UHURU 2023 HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU












# WANAFUNZI VIONGOZI WA KLABU ZA WATOTO MKOA WA ARUSHA WATEMBELEA BUNGE KUJIFUNZA







Viongozi wa klabu na mabaraza ya watoto kutoka Halmashauri tatu za Mkoa wa Arusha, Meru, Karatu na Jiji Wakifuatilia Bunge

Viongozi wa klabu na mabaraza ya watoto kutoka Halmashauri tatu za Mkoa wa Arusha, Meru, Karatu na Jiji wakiambatana na viongozi toka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wataalamu wa Mkoa wa Arusha na Halmashauri pamoja na Viongozi na watumishi toka Shirika la SOS CHILDREN'S VILLAGE wamepata fursa ya kufuatilia shughuli za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo tarehe 13/06/2023 Viongozi hao wa klabu za Watoto ikiwa ni sehemu ya ziara ya mafunzo ya siku tano jijini Dodoma. wameshuhudia namna muhimili wa Bunge unavyoendesha shughuli zake ambapo pia watapata fursa ya kutembelea chuo cha Dodoma, Mji wa Serikali mtumba na kushiriki maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika ambayo inahitimishwa Kitaifa Mkoani Dodoma tarehe 16/06/2023. Hilda Mgomapayo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, ambaye ni mratibu wa dawati ulinzi na Maendeleo ya Mtoto amesema Serikali kupitia Ofisi, ya Rais TAMISEMI inasimamia na kuratibu uundwaji wa Klabu hizi ikiwa ni utekelezaji wa sera ya Mtoto, Sheria za Nchi na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa. Ikumbukwe shirika la SOS CHILDREN'S VILLAGE Kwa kushirikiana na Serikali kupitia Mkoa wa Arusha na Halmashauri waliwezesha kuundwa Kwa klabu za watoto mashuleni zimekuwa msaada na jukwaa muhimu la kuwasilikiliza watoto lakini pia kupokea changamoto zao na kuzifanyia kazi.

# BAADHI YA WADAU KUTOKEA HALMASHAURI ZA ARUSHA WANAOWAWEZESHA WANAFUNZI WAKISALIMIA BUNGENI



Ikumbukwe shirika la SOS CHILDREN'S VILLAGE Kwa kushirikiana na Serikali kupitia Mkoa wa Arusha na Halmashauri waliwezesha kuundwa Kwa klabu za watoto mashuleni ambazo zimekuwa msaada na jukwaa muhimu la kuwasilikiliza watoto lakini pia kupokea changamoto zao na kuzifanyia kazi Awali akizungumzia umuhimu wa ziara hiyo , Afisa ustawi wa jamii Mkoa wa Arusha ndugu Denis Mgiye amesema Watoto watapata uzoefu na kuongezewa ujasiri wa namna ya kuendesha vikao vyao na kuibua masuala mbali mbali yanayohusu ulinzi na usalama wa Mtoto..

PICHA YA PAMOJA YA WADAU MBALIMBALI PAMOJA NA VIONGOZI NJE YA JENGO LA BUNGE DODOMA



# DC ARUMERU ASHIRIKI KATIKA UJENZI WA MADARASA KIJIJI CHA KALOLENI

Wananchi wa Kijjiji cha Kaloleni Kata ya Majengo Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Wilayani Arumeru wamemshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa Milioni 106.3 za ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na vyoo vya wanafunzi wa kike matundu manne. Wananchi wamesema hayo wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe.Emmanuela Kaganda ya kukagua utekezaji wa miradi ya BOOST katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Akizungumza kwa niaba ya Wananchi wa Kaloleni Diwani wa Kata ya Majengo Mhe.Bernard Kivondo amemshukuru Rais.Samia kwa kuendelea kutoa fedha za maendeleo katika shule ya Msingi Kaloleni kwa awamu ambapo Serikali kupitia TASAF ilitoa milioni 74 za ujenzi wa Vyumba viwili vya madarasa na ofisi, pia ilitoa milioni 12.5 za ukamilishaji wa chumba cha darasa na sasa imetoa Milioni 106.3 fedha za mradi wa BOOST kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na vyoo Aidha, Mhe. Kivondo amesema Wananchi wa Kaloleni wamehamasika na maendeleo yanayofanywa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na wanashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi kwa kuchangia nguvu kazi ambapo viton goji vya kijiji cha Kaloleni vinau taratibu wa zamu ya nguvu kazi. Awali, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda amesema Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipanga kuwaletea wananchi wake maendeleo kwa ngazi zote ambapo katika sekta ya elimu msingi imetoa milioni 961.5 fedha za BOOST kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu katika shule za msingi ili kuhakikisha watoto wa Kitanzania wanapata elimu bora katika mazingira rafiki. Aidha, Mhe. Kaganda ameelekeza miradi inayotekelezwa kuwa na viwango na ubora sambamba na kutekelezwa kwa wakati.









DC Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda Akishiriki katika Ujenzi wa Madarasa Kijiji cha Kaloleni

Ilani ya CCM ya mwaka 2020, Sura ya tatu ibara ya 78 inaeleza "CCM inatambua kuwa rasilimaliwatu ndio nyenzo muhimu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha CCM inaamini kuwa elimu bora ndio nyenzo muhimu ya kujenga ,kulea na kuendeleza rasilimaliwatu ili ziweze kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa Taifa na maendeleo ya jamii kwa ujumla"

# WANANCHI ARUMERU WASHIRIKI KUTEKETEZA HEKARI 60 ZA BANGI

Wananchi wa Kijiji cha kisimiri juu, Kata ya Uwiro Halmashauri ya Wilaya ya Meru, washiriki operesheni endelevu ya kuondoa kukamata na kuteketeza zao haramu la madawa ya kulevya aina ya bangi inayoendeshwa na Kamati ya ulinzi na usalama Wilayani humo. Wakizungumza Mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda, wakati wa operesheni hiyo shirikishi Wananchi hao ambao wameshiriki kung'oa na kuteketeza bangi wamesema, katika Kata hiyo kuna fursa nyingi za kilimo ambapo wameahidi kuacha kilimo cha bangi na kulima mazao halali ya chakula na biashara.

Akizungumza kwa niaba ya Wananchi hao Mwenyekiti wa kijiji cha κisimiri Juu Mayani Lukumay ameiomba Serikali kuboresha miundombinu ya Barabara kufika kijijini hapo kwani wananchi wanaweza kulima mazao ya viazi, njegere,pareto lakini changamoto kubwa ni namna ya kuyafikisha mazao hayo sokoni. Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda amesema katika operesheni hiyo wamefanikiwa kukamata gunia 10 za bangi kavu, kukusanya mbegu za bangi kg 30 na kuteketeza hekari 60 za mashamba ya bangi mbichi.

Aidha, Mhe. Kaganda ametoa siku saba kwa wananchi kisimiri juu, Kisimiri chini na maeneo yote kinapofanyika kilimo cha zao hilo haramu kuhakikisha wanang'oa na kuteketeza mmea wa bangi kwenye Mashamba yao kwani baada ya siku hizo yeyote ambaye shambalake litakutwa na mmea huo sheria itachukua mkondo wake. Awali Viongozi wa kimila wa kijiji hicho wamewataka vijana kuachana na kilimo cha bangi kwani







Pichani ni Wananchi wa Kisimiri Juu wakishirikiana na Mkuu wa wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda katika zoezi la kuteketeza Bangi

# UTATUZI WA MIUNDOMBINU CHAKAVU KUELEKEA MIAKA 59 YA MUUNGANO, DC ARUMERU AZINDUA VYUMBA VYA MADARASA

Kuelekea maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, wanafunzi wa Shule ya Msingi Kikwe iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Meru ,Wilayani Arumeru waondokana na changamoto ya uchakavu wa vyumba vya madarasa baada ya Serikali ya Dkt.Samia Suluhu Hassan kutoa shilingi Milioni 60 za ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa pamoja Samani (Meza na viti 50 kwa kila darasa) shuleni hapo Akizundua vyumba hivyo vya Madarasa, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda amesema Wilaya ya Arumeru inaishukuru Serikali kwani kuelekea miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Serikali ya awamu ya sita imetoa fedha nyingi katika sekta za Elimu,Afya ,Kilimo nk Mhe.Kaganda ameipongeza Serikali ya Dkt.Samia kwani imehakikisha wanafunzi wanasoma kwenye vyumba vya kisasa vya madarasa vyenye viti na Meza, Umeme, vigae (tiles) ambapo ametoa wito kwa Walimu kusimamia utunzaji wa miundombinu mashuleni ili kuwa na tija zaidi. Vilevile Mhe.Kaganda amewapongeza viongozi wote walioshiriki kusimamia ukamilishaji wa mradi wa huo, ambapo ametumia jukwaa hilo kuwakumbusha tumia jukwaa hilo kuwakumbusha wakulima kulima mazao ya muda mfupi kuzingatia taarifa za mamlaka za Hali ya Hewa, na kubainisha kwa Sasa mbolea inapatikana Wilayani Humo . Mhe.Daniel Kaaya ambaye ni Diwani wa Kata ya kikwe amesema ndani ya miaka miwili wamefanikiwa kupata miradi mingi ambayo kila kijiji cha kata ya kikwe kimepata mradi. kwa upande wao wazazi na Wanafunzi wameishukuru Serikali kutoa fedha za ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa kwani kwa Sasa wanafunzi watasoma katika mazingira mazuri na rafiki.









PICHANI NI MKUU WA WILAYA YA ARUMERU MHE. EMMANUELA KAGANDA AKIZINDUA VYUMBA VYA MADARASA

# DC ARUMERU AHIMIZA WANANCHI WA MERU KUPANDA MITI KANDO YA VYANZO VYA MAJI









Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Emmanuela Kaganda pamoja na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Meru Mwl. Zainabu J. Makwinya wakipanda Miti

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Emmanuela Kaganda ametoa wito kwa wananchi kutunza vyanzo vya maji na mazingira ambapo pia amewataka wanaofanya shughuli za kibinadamu katika milima kuacha mara moja kwani Serikali wilayani humo haitowafumbia macho. Mhe.Kaganda amesema hayo wakati akiwaongoza wananchi-i wa Kata ya Mbuguni Halmashauri ya Meru, kupanda miti kwenye kingo za korongo la mto Nduruma ambalo Serikali ya awamu ya Sita ikiongozwa na Rais.Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitoa zaidi ya Milioni 200 za kufukua korongo hilo na kutatua changamoto ya mafuriko iliyokuwa ikiwakabili wananchi wa Kata hiyo ya Mbuguni na Shambarai Burka..

Mhe.Kaganda amesema Wilaya ya Arumeru imebarikiwa kuwa na vyanzo Vingi vya maji vinavyoanzia milimani, hivyo wananchi hawana budi kuvitunza kwa manufaa yao na manufaa ya wengine " Wazee wetu walitunza vyanzo hivi nasi tunapaswa kuvitunza kwa ajili ya kizazi kijacho" amehimiza Mhe Kaganda

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl Zainabu J. Makwinya amesema Halmashauri inahakikisha inaunga mkono juhudi za Serikali katika agenda ya utunzaji mazingira na vyanzo vya maji, ambapo awali kupitia mapato yake ya ndani Waheshimiwa madiwani waliridhia kutoa Milioni 26 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwenda kuchimbua Korongo hilo la mto Nduruma kutunza vyanzo vya maji vilivyopo kwani hakuna mbadala wake ambapo amebainisha Bonde la

Nao Waheshimiwa Madiwani wa Kata za Shambarai na Mbuguni ambazo awali zilikuwa zikisumbuliwa na mafuriko wameishukuru Serikali kufukua Korongo hilo na kutoa wito kwa wananchi kuendelea kutunza vyanzo vya maji. Tito Kitomari kutoka Bonde la Pangani ametoa Wito kwa jamii kutunza vyanzo vya maji vilivyopo kwani hakuna mbadala wake ambapo amebainisha Bonde la Pangani kuendelea kushirikiana na jamii. Pangani kuendelea kushirikiana na Jamii na Serikali katika utunzaji wa vyanzo vya maji.











# ZIARA YA KAMATI YA FEDHA ,MIPANGO NA UTAWALA. 19/04/2023



Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mhe. Jeremia Kishili na Pembeni yake ni Makamu Mwenyekiti Pamoja na wajumbe wengine kwenye ziara

Wajumbe wa kamati ya utawala, fedha na mipango wakiongozwa na mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mhe.Jeremia Kishili wamefanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, katika ziara hiyo wananchi wa kata zilizotembelewa wametuma Salamu kwa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi za maendeleo kwenye maeneo yao "tunashukuru Kata yetu ya Kikatiti tumepokea Miradi mingi ,zahanati imekamilika,nyumba ya mtumishi imekarabatiwa, uboreshaji sekta ya Elimu tumenufaika na leo tunafuraha Madiwani mnakagua ujenzi wa Uzio kwenye soko letu la kikatiti "Amesema Nuru Mkazi wa Kikatiti Ikumbukwe Baraza la Halmashauri linaongozwa na Mhe.Kishili linaweka historia kuwapelekea wananchi wa Pembezoni maendeleo ambapo limetoa shilingi Milioni 400 za mapato yake ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ya kikatiti









# MERU YATOA BARAKA KWA WANAMICHEZO WA UMISSETA 2023

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl Zainabu Makwinya ameitakia kheri timu ya Halmashauri hiyo ya wanafunzi wa shule za Sekondari itakayoshiriki mashindano ya Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) 2023 ngazi ya Mkoa yatakayofanyika Mji wa Karatu kuanzia tarehe 4 hadi 6 Juni 2023. Akiagana na wanamichezo hao wanaoelekea kambini Mjini Karatu kwa maandalizi, Mwl.Makwinya amewataka kuzingatia mafunzo ya makocha ,kujiamini, kujiandaa na kujituma ili kuiletea Halmashauri ushindi ambapo pia amewapongeza wazazi wanaotoa fursa kwa watoto kushiriki michezo ni fursa' amesisitiza Makwinya Naye, Marcel Itambu Afisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Meru, amesema timu hiyo ya wachezaji 125 na walimu 11 inayokwenda kambini ipo vizuri kwani wamefunzu mashindano ngazi ya Kata na Kanda katika uundaji wa timu ya Halmashauri. Aidha katika mashindano ya UMISSETA 2023 Michezo itakayoshiriki ni Mpira wa miguu wavulana na wasichana, Mpira wa kikapu wavulana na wasichana, Mpira wa mikono wavulana na wasichana, Mpira wa wavu wavulana na wasichana, Mpira wa Pete,Mpira wa miguu maalum,Riadha,Fani za ndani (Ngoma, kwaya, hip-hop),Mpira wa meza. Ikumbukwe UMISSETA 2022 timu ya Halmashauri ilinyakua vikombe tisa katika michezo mbalimbali na wanamichezo 6 walivalishwa medali za ushindi. Meru tupo vizuri na Kazi iendelee







Baadhi ya Picha za Wanamichezo wa UMISETA Wakiwa njee ya Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Meru na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru



# JARIDA LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU LINALOZUNGUMZIA MAENDELEO MBALIMBALI YA HALMASHAURI LINALOTOKA KILA BAADA YA MIEZI MITATU (KOTA)

**APRILI - JUNI**

**@2023**

HALMASHAURI YA WILAYA MERU DISTRICT COUNCIL